



## Ewe Mola wangu, hakika mimi ni mwanadamu, basi yeyote katika Waislamu niliyemtukana au kumlaani au kumpiga kwa mjeledi, basi hilo lifanye kwake kuwa ni utakaso na huruma

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Ewe Mola wangu, hakika mimi ni mwanadamu, basi yeyote katika Waislamu niliyemtukana au kumlaani au kumpiga kwa mjeledi, basi hilo lifanye kwake kuwa ni utakaso na huruma".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Aliomba Mtume rehema na amani ziwe juu yake akasema: Ewe Mola wangu, hakika mimi ni mwanadamu, hivyo basi, muumini yeyote niliyemuudhi au kumtukana au kumshutumu, au kumlaani, na nikamuomba kufukuzwa katika rehema yako, au nilimpiga mjeledi au kipigo chochote, basi lifanye hilo kwake kuwa ni utakaso na ibada na twahara na kafara na rehema utakayomhurumia kwayo.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/65812>

